

I

## KISWAHILI KIDATO CHA TATU

### MUHULA 1

JINA.....NAMBARI.....

**KARATASI YA FASIHI**

**102/3**

**MUDA: 2½**

**MAAGIZO:**

- **Jibu maswali manne**
- **Swali 1 ni lazima**
- **Jibu maswali matatu kutoka kwa sehemu zilizobakia**

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

<b>SWALI</b>	<b>UPEO</b>	<b>ALAMA</b>
<b>SEHEMU YA A</b>	<b>20</b>	
<b>SEHEMU YA B</b>	<b>20</b>	
<b>SEHEMU YA C</b>	<b>20</b>	
<b>SEHEMU YA D</b>	<b>20</b>	
<b>JUMLA</b>	<b>80</b>	

*Kila mtahiniwa lazima aangalie kama kurusa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo*

**SEHEMU YA A:USHAIRI**

**1. Soma shairi na kisha uyajibu maswali yafuatayo:-**

1. Ni sumu, sumu hatari  
Unahatarisha watoto  
Kwa ndoto zako zako leweshi  
Za kupanda ngazi  
Ndoto motomoto ambazo  
Zimejenga ukuta  
Baina ya watoto  
Na maneno laini  
Ya ulimi wa wazazi
2. Ni sumu, sumu hasiri  
Unahasiri watoto  
Kwa pupa yako hangaishi  
Ya kuwa tajiri mtajika  
Pupa pumbazi ambayo  
Imezaa jangwa bahili  
Badala ya chemichemi  
Ya mazungumzo na maadili  
Baina ya watoto na mzazi
3. Ni sumu, sumu legezi  
Unalegeza watoto  
Kwa mazoea yako tetanishi  
Ya daima kunywa 'moja baridi'  
Mazoea mabaya ambayo yanafunga katika klabu  
Hadi saa nane usiku  
Huku yakijenga kutofahamiana  
Baina ya watoto na mzazi
4. Ni sumu, sumu jeruhi  
Unajeruhi watoto kwa pesa,  
Kwa mapenzi yako hatari  
Ya kuwaliwaza watoto kwa pesa  
Zinawafikisha kwenye sigara na ulevi  
Na kisha kwenye madawa ya giza baridi  
Barabara inayofikisha kwenye giza baridi la kaburi la asubuhi

**Maswali**

- (a) Pendekeza kichwa kwa shairi hili. **(alama 1)**
- (b) Fafanua maudhui ya shairi hili. **(alama 2)**
- (c) Ni kwa njia gani kinachozungumziwa kinajenga ukuta? . **(alama 2)**
- (d) Dondoa tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi na uzitolee mfano **(alama 4)**
- (e) Eleza umbo la shairi hili. (alama 3)
- (f) Uandike ubeti wa nne kwa lugha nathari. **(alama 4)**
- (g) Eleza maana ya vifungu hivi vilivyotumika katika shairi . **(alama 4)**
  - (i) Giza baridi
  - (ii) Yanakufunga katika klabu

**SEHEMU YA B: KIDAGAA KIMEMWOZEA**

2. Jadili umuhimu wa mbinu ya majazi kwa kurejelea jina Sokomoko. **(alama 20)**
3. “alisimama jadidi na kuwatazama hawa watu wawili waliosimama wima kutetemeka kama waliokuwa wamepigwa na dhoruba ya theluji.”
- a) fafanua muktadha wa dondoo hili **(alama 4)**
  - b) taja mbinu mbili za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hii.**(alama 4)**
  - c) onyesha umuhimu wa ‘anayesimama jadidi’ katika kuijenga riwaya hii.**(alama 12)**

**SEHEMU YA C:MSTAHIKI MEYA**

4.“..wewe hukubaliani na chochote siku zote. Kauli yako ndiyo waiona kuwa yenye hoja inayoistahili kufuatwa.”

- a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**
- b) Eleza nyakati zingine ambapo wahusika hawa wawili walitofautiana.**(alama16)**

5.Taja na ueleze njia anazozitumia Meya katika kuuendeleza uongozi wake. **(alama 20)**

**SEHEMU YA D:DAMU NYEUSI NA HADITHI ZINGINE**

6.“ si udufu kitu gani,mtu aache kutukia nyayo za kweli.....”

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama 4)**
- b) Jadili hulka na umuhimu wa msemaji **(alama 16)**

7.Kwa kulejelea hadithi tofauti katika diwani ya Damu nyeusi na hadithi nyingine, jadili maudhui haya: **(alama 20)**

- a) Ubaguzi

- b) Ndoa
- c) Umaskini

**SEHEMU E:FASIHI SIMULIZI**

8. a) Taja na ueleze sifa za mtambaji bora katika fasihi simulizi. **(alama 10)**

b) Nyimbo zina wajibu gani katika jamii. **(alama 4)**

c) i) Eleza maana ya vitendawili. **(alama 2)**

ii) Onyesha sifa za kitendawili. **(alama 4)**

9. a) Taja na ueleze aina nne kuu za hadithi **(alama 8)**

b) Eleza mbinu tatu ambazo mtambaji anaweza kutumia kuishirikisha hadhira yake. **(alama 6)**

c) Fafanua vipera vifuatavyo vya fasihi simulizi. **(alama 6)**

i) Majigambo

ii) Mivigha

iii) Lakabu